Ukweli Hauna Kutu

# Pambazuko

Toleo Namba 020 Jumatatu Novemba 21-27, 2022

# Nani mwizi wa laptop 13?

Uk.10

*•Ni za abiria wa Precision Air iliyopata ajali*

## Bashiru hawezi kuaminika tena

Uk. 5




## Maji kuibua mgogoro

Uk.11

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

# Maji ya ardhini yaachwe kwanza

WAKAZI wa Jiji la Dar es Salaam na viunga vyake, wako katika kero kubwa ya kupatikana maji kwa takribani miezi miwili sasa.

Kila familia inahaha kupata maji kwa ajili ya matumizi; matajiri wanaonekana wakigombea magari yenye kusambaza maji majumbani na wenye uwezo mdogo wanapigana vikumbo kwenye mashimo pembezoni mwa barabara yanayotunza maji machafu.

Hawa wote, bila kujali uwezo wao wa kiuchumi, wamo katika mtanziko mkubwa wa kupata maji. Ni kutokana na umuhimu wake kwa binadamu – kama ilivyo kwa hewa, hakuna mwenye unafuu. Wote wanateseka.

Kadhia hii ya kukosekana maji Dar es Salaam, kimsingi imevua nguo viongozi wakuu wa serikali, siyo katika jiji hilo mahsusi katika kukuza uchumi wa Tanzania, bali taifa zima, hasa wale watendaji wa wizara inayohusika na masuala ya maji.

Mbali na viongozi hao, watendaji wa mamlaka ya maji katika jiji hilo, nao wameonekana "wapowapo tu" – wakiwa na kazi ya kuhimiza malipo ya ankara za maji, huku suala la kuhakikisha maji yanapatikana kwa uhakika, likionekana kupewa kisogo.

Wananchi nao, ukosefu wa maji umewaumbua kwa kuwatambulisha kwamba, wakazi wengi wa jiji hilo ni wepesi mno katika kutunza msaada wa kesho - siyo katika maji tu, bali hata katika maeneo mengine.

Sisi katika Pambazuko tumewashangaa viongozi wetu wa serikali, wale wa jiji la Dar es Salaam ambao wamedhihirika kabisa kuwa uwezo wao wa kupambanua mazingira na kupambana nao, unatia shaka.

Tumewaona na kuwasikia baadhi ya viongozi hao, badala ya kuja na mbinu za kutatua tatizo hilo, wao wanakimbilia kumsingizia Mungu; eti kwamba ndiye ameleta ukame huu. Hii ni akili gani ya kumsingizia Muumba kwa matatizo yetu ambayo tungeweza kuyafanyia kazi kabla hayajawa kero kubwa.


Hivi hawa viongozi pamoja na wataalamu wetu wa maji, hawakujua kwamba kufikia muda Fulani maji ya Dar es Salaam, yanaweza yasitoshe, hivyo kuhitajika mbinu za kisasa kuhakikisha maji ya uhakika anapatikana.

Inashangaza zaidi kusikia wataalamu wetu wanamuongopea hadi mkuu wa nchi kwamba ukosefu wa maji katika jiji hilo umesababishwa na ng'ombe 5000 kuvamia mto na kunywa maji hayo.

Eti kila ng'ombe anakunywa lita 45 kwa siku, wakati wanasahau kwamba wapo Wachina wamepewa ruhusa ya kukinga maji ya mito kunyweshea mazao yao na wanatumia lita milioni moja kila siku – hawa hawasemwi isipokuwa ng'ombe. Ajabu!

Mbali na "wakubwa" hawa, wananchi nao lazima wabebe lawama ya kukosekana kwa maji. Wamekuwa chanzo kikubwa cha kuharibu mazingira, ambayo ni chanzo kikuu cha uhakika wa maji.

Hata hivyo, pamoja na yote, Pambazuko inahimiza - chondechonde, kuvuna maji ya ardhini kuachwe kwanza kwa sasa. Yatatuokoa pakubwa baadaye.




## NUKUU



*"NAPENDA kuwaambia wale wanaodhani siasa haiwahusu, moja ya madhara ya kukataa kujihusisha na siasa ni kwamba utaongozwa na watu uliowazidi akili na hata busara, na kwa upungufu wao wa akili watafanya uamuzi wa kila kitu kinachohusu maisha yako leo na hata kesho"-* ***Plato.***

# Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

# Ni muda muafaka kuacha VX-V8

**Na Scovya MANASE**

KUNA kila dalili kwamba Tanzania itakabiliwa na hali ya ukame, upungufu wa chakula na zaidi sana kuwepo kwa ongezeko la joto kwa mwaka ujao.

Dalili hizo zinabebwa na mazingira ya sasa na hali ya hewa ambayo inaonyesha kabisa kutokuwepo kwa unafuu katika siku za hivi karibuni.

Majanga yanayotokana na kuvurugika ama kuvurugwa kwa mazingira kutokana na kazi za binadamu, yanaeleweka, hivyo ni wajibu wa kujipanga ili kukabili lolote linaloweza kutokea ili kupungzua madhara.

Moja ya njia za kujipanga ni kuhakikisha kuwa serikali inabana maftumizi yake kuanzia sasa na isisubiri kutokea kwa majanga hayo ndipo mianze "kukimbiakimbia."

Eneo moja ambako serikali inaweza kukata matumizi na kupata ziada inayoweza kuhamishiwa kwenye eneo jingine, ni kwenye ya magari ya serikali.

Kwa mujibu wa hotuba ya bajeti ya serikali ya mwaka 2022/23, iliyosomwa Juni mwaka huu na Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, serikali ina magari 15,742, pikipiki 14,047, na mashine 373.

Alifafanua kwamba, gharana za ununuzi, mafuta na ukarabati wa vyombo hivi ni zaidi ya Sh. bilioni 558 kwa mwaka. Kwa miaka mitano, bajeti hii ni zaidi ya Sh. trilioni 2.7.

Kama itachukuliwa kwamba ujenzi wa darasa moja la wanafunzi ni Sh. milioni 250, basi fedha hiyo ingejenga madarasa 111,690.

Kama tukichukulia kwamba ujenzi wa zahanati moja kijijini ni Sh. milioni 100, basi fedha hiyo ingejenga zahanati 27,922. Tanzania inavyo vijiji 12,319. Hivyo, fedha hiyo ingejenga zahanati mbili katika kila kijiji.

Gari jipya la Toyota Landcruiser VX, linapatikana kwa wastani wa Sh. 400.



*Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba,*

Endapo Tanzania itaachana na ununuzi wa magari yenye bei "mbaya" na kuagiza yenye nusu bei ya hayo "maVX," serikali itaokoa kiasi kikubwa cha fedha ambacho kinaweza kuelekezwa maeneo muhimu zaidi kwa ustawi wan chi na wala siyo kwa viongozi pekee.

Kwa hiyo sasa, wakati umefika kwa serikali kufanya uamuzi mgumu wa kukata gharama za uendeshaji wake kwa kuchagua aina ya magari yanayoendana na pato la taifa na kwa kujali zaidi maslahi ya wengi dhidi ya "raha" za watawala.

Pia kama yapo magari ambayo yanaweza kuuzwa kwa wananchi, basi ifanyike hivyo na fedha zinazopatikana zitunzwe kwa ajili ya kusaidia kipindi kigumu kinachotarajiwa kuwepo.

Haya yamewezekana kwa mataifa mengi, hata yaliyoendelea ambako uendeshaji wa serikali unakuwa nafuu zaidi, huku nguvu kubwa ikielekezwa kwenye neema ya kila mtu.

# Bashiru hawezi kuaminika tena

**Na John PAMBALU**

VYOMBO vya habari na mitandao ya jamii wiki iliyopita vilimnukuu Dkt. Bashiru Ally, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Katibu Mkuu Kiongozi wakati wa utawala wa Rais John Magufuli, akikosoa wanaosifu na kuupongeza uongozi wa sasa wa Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza katika hafla iliyoandaliwa na mtandao wa wakulima wadogo (Mviwata) alisema; "sauti yenu wakulima, iwatishe wanyonyaji wenu, kama hatujafikia hatua hiyo na kutisha watawala, bado tutakuwa hatujafikia malengo."

Bashiru aliendelea kusema; "hatutakuwa tofauti na mawakala wao, wanaowapamba na wakati mwingine kuwadanganya kwamba wanaupiga mwingi, Mviwata mkifika hatua ya kusema mnaupiga mwingi, basi uhai wenu uko mashakani."

Maneno ya Dkt. Bashiru yanaibua mambo kadhaa katika hoja zake na kwamba yanabeba mambo mazito ambayo hayapaswi kuchukuliwa kwa wepesi.

Kwamba Dkt. Bashiru anataka wakulima waungane kiasi cha kuwa tishio kwa watawala na mawakala wao.

Kwamba watawala wanao watu wanaowapamba, wakati mwingine wapambe wamekuwa waongo kwa kuwadanganya watawala kuwa wanaupiga mwingi kumbe waongo.

Kwamba ustawi wa jamii uko shakani kama itajikita katika kusifu na kushukuru watawala bila ya kwua na nafasi ya kuhoji.

Binafsi sina pingamizi na hoja za Dkt. Bashiru. Nina tatizo na uhalali wa kisiasa na wa kijamii (uhalali wa kimaadili ) msomi huyo aliyegeuka kuwa mwanasiasa mbabe wakati wa utawala wa Magufuli.

Kauli za Dkt. Bashiru anayezungumza leo vizuri, vinamtofautisha na yule aliyeonekana kutisha kila mtu na kujifanya mbabe kwa lengo la kumfurahisha aliyemteua na kumpa majukumu makubwa. Aliiga kila staili aliyokuwa nayo Magufuli na hakika ilimtofautisha na usomi wake.



*Dkt. Bashiru Ally,*

Bado kuna maswali - nini hasa kimembadilisha Dkt. Bashiru ajitokeze leo kukemea mambo ya kusifu na kuabudu watawala - mambo ambayo yalikuwa kama sala na utamaduni wa kawaida kwa wasaidizi wote wa Magufuli? Nini kinamfanya aone sifa zilistahili kwa kiongozi wa awamu ya tano na siyo kwa Rais Samia?

Katika mazingira yaleyale ya kusifu na kumwabudu mtawala, mkuu wa mkoa mmoja nchini aliwahi kusema kwamba Mungu amshukuru Magufuli kwa uchapa kazi wake.

Kama hiyo haitoshi, profesa mmoja ambaye alikuwa waziri aliwahi kumuita Magufuli kuwa - "Mheshimiwa Mungu, na waziri mwingine akatamka "Magufuli ni zaidi ya Yesu na mitume" – hizi ni kufuru kubwa ambazo zilikuwa zikiimbwa na wengi. Hawa ni wachache walionaswa na vyombo vya habari.

Dkt. Bashiru anakerwa nini endapo wapo wenzake wanaendeleza hayo aliyoyaiga na kuyalea hadi alipoondolewa kwenye nafasi za juu na kukosa tonge?

Heri Dkt. Bashiru akae kimya! Kwani haaminiki tena.

***Mwandishi ni Mwenyekiti wa Baraza la Vijana wa Chadema (Bavicha).***

# Atetea PW, alaani uwanja, uokozi

**Na Shabaan LULELA**

ENDAPO kungekuwa na taa za kuongoza ndege katika uwanja wa Bukoba, huenda rubani asingelazimika kutua Ziwa Victoria na kusababisha vifo vya watu 19 na wengine 24 kuokolewa.

Mbali na hivyo, tofauti na mtazamo wa baadhi ya watu kuwa baadhi ya ndege za Kampuni ya Precision Air (PW), ikiwamo ndege iliyopata ajali Novemba 6, mwaka huu, zimezeeka; ndege hiyo ilikuwa bado mpya kwa mujibu wa "umri" wa chombo hicho kuwa angani.

Msimamo huo umetolewa na Bubelwa Bandio, mtaalamu wa uongozi katika usafiri wa anga ambaye amehudumu katika idara kadhaa, ikiwamo kuongoza ndege na maeneo mengine nchini Marekani kwa miaka 17, huku miaka mitano akiwa kiongozi wa idara anayoitaja kuwa "nyeti."

Akizungumza na Pambazuko wiki iliyopita, mtaalamu huyo ambaye ni Mtanzania kwa kuzaliwa, akifanya shughuli zake Jiji la Washington, amesema ameshangazwa kubaini kwamba uwanja huo hauna taa za kuongoza ndege kutua na hata kuruka.

Bandio anaeleza kuwa katika mazingira na hali ya hewa ya Bukoba kubadilika badilika, taa za kuongoza ndege hazipaswi kuzimwa – kama zipo na kuwa uwepo wake humsaidia zaidi rubani kutua na kurusha ndege.

"Kama taa zingekuwepo, kama rubani aliamua kutua, angeweza kwa kuongozwa na taa, kwani huonekana hata wakati wa mvua, ukungu na giza, naambiwa hazipo, sasa hapo uone namna uzembe ulivyochangia kuua watu 19, ambao wangeweza kuokoka ama kuokolewa," ameongeza mtaalamu huyo.

Mtaalamu huyo anatetea ubora wa ndege aina ya ATR 42-500, ambazo hutengenezwa nchini Ufaransa, zikiwa na baadhi ya vifaa muhimu kutoka Italia kwa maelezo kwamba ni bora na



kwamba hazina historia ya kuharibika mara kwa mara. Kampuni ya ndege ya Aérospatiale kutoka Ufaransa (sasa Airbus) kwa ushirikiano na kamouni ya Itali Aeritalia (sasa Leonardo S.p.A.) ndiyo watengenezaji wa ndege hiyo ya Precision Air.

Anasema ndege iliyopata ajali ilikuwa na urefu wa mita 22.7 na kimo cha urefu unaofikia mita 7.6, huku ikiwa na uwezo wa kubeba abiria hadi 43 na kwamba ilikuwa na umri wa miaka 12, hivyo "ilikuwa bado mpya kwa mujibu wa umri wa ndege zinazopaswa kuendelea kufanya kazi."

Bandio anasema kuwa abiria waliopoteza maisha yao, walifariki dunia kutokana na uzembe zaidi kwa watendaji – hasa kitengo cha uokozi katika uwanja wa Bukoba, kwa kuwa walishindwa hata kufika haraka kuokoa.

"Watendaji wa idara ya usalama na uokozi katika uwanja huo, baada ya ndege kutua majini, walipaswa kuwa wa kwanza kufika, lakini walionekana eneo la ajali baada ya karibu nusu saa, huku ikishangaza kwamba wavuvi waliotumia mtumbwi usiokuwa na injini uliwawahi, ni bahati mbaya sana," anaongeza kwa uchungu.

# Lissu amkomalia Samia mikutano

Na Tryruckia MFINANGA

KITENDO Rais Samia Suluhu Hassan kuendelea kuzuia mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa - hasa upinzani, ni dalili ya kuimarisha udikiteta anaohubiri kupinga.

Huo ni msimamo wa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Maendeleo na Demokrasia (Chadema), Tundu Lissu na kwamba anamtaka Rais Samia kuacha kuzuia mikutano hiyo kwani ndiyo uhai wa vyama vya siasa makini.

Akizingumza na Pambazuko kutoka Brussels, Ubeligiji anakoishi kwa sasa, Lissu alisema Rais Samia bado anaonekana "kubeba" baadhi ya hulka za mtangulizi wake, John Magufuli, hasa katika eneo la demokrasia.

"Sisi Chadema ni chama cha mikutano ya hadhara kihistoria, chama chetu kimekua sana tangu miaka ya 2005 kwa sababu ya kwenda kwa wananchi kupitia njia ya mikutano ya hadhara, lakini tumezuia kwa miaka saba sasa, kwa kuwa tu serikali inataka chama kife," anasema Lissu.

Akiwa kiongozi wa Tanzania, Rais Magufuli baada ya kuingia madarakani, Novemba 2015, alipiga marufuku mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa, akidai kuwa ni kupoteza muda wa wananchi, kwani muda mwingi unapaswa kutumika kuzalisha mali na siyo siasa. Magufuli alifariki dunia mwaka Machi 17, 2021.

Lissu anasema Rais Samia kuendelea kuminya uhuru wa vyama vya siasa na kujieleza, ni dalili mbaya kwa ustawi wa Tanzania na watu wake na kwamba ni kuendeleza "mabaya ya Mabufuli" anayoeleza 'kuyazika.'

Anasema ni dhahiri shahiri kwamba sehemu kubwa ya umaarufu na ushawishi wa Chadema umetokana na kazi kubwa iliyofanyika kujenga imani kwa Watanzania kupitia mikutano ya hadhara.

Lissu anasema woga aliokuwa nao Magufuli kwa Chadema, ndiyo unaendelezwa na Rais Samia kwa kuzuia chama hicho kikuu cha upinzani kisifanye kazi zake.



*Tundu Lissu*

Hata hivyo, anabainisha kwamba pamoja na kunyimwa haki ya mikutano ya hadhara, imani ya Watanzania kwa Chadema imeedelea kuimarika na kupatikana kwa wanachama wapya kila siku.

Chadema kwa sasa inatumia zaidi mikutano ya ndani, makongamano mbalimbali kujiimarisha.

Lissu anatamba kwamba ndani ya mazingira magumu ya kuendesha siasa za upinzani Tanzania, bado Chadema ni bora zaidi katika kuhamasisha wananchi na wafuasi wake kuliko vyama vyote nchini, kikiwamo chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Anaeleza kuwa endapo chama chake kitaruhiswa kufanya mikutano ya hadhara, nguvu za Chadema zitakuwa maradufu na kutishia utawala wa CCM na serikali yake.

"Hili zuio haramu siku likiondoka, tutakuwa na nguvu kubwa mno, moto utakuwa mkubwa zaidi na hili ndiyo linawatisha CCM na serikali yake, hawana jingine," anaongeza Lissu amnaye ni wakili wa Mahakama Kuu Tanzania.

# Uhakiki wa uwiano wa mamlaka

**Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA**



NGUZO ya nne ya demokrasia ni uhakiki wa uwiano wa mamlaka (checks and balances). Nguzo hii hutumika pia katika uongozaji wa taasisi mbalimbali nje ya serikali.

Katika mijadala iliyotangulia nimeitaja nguzo hii kwa kupitia, lakini hapa nataka niseme zaidi kidogo. Katika katiba za mataifa yanayofuata mfumo wa utawala wa kidemokrasia hutokea mara nyingi kwamba katiba zao hugawa serikali katika mihimili mIkuu mitatu: bunge, utawala na mahakama. Hivi ndivyo ilivyo hata katiba ya Tanzania.

Kila mhimili unapewa mamlaka zake na wakati huohuo kuhakikisha kwamba yaliyomo katika mhimili mmoja hayamo katika mwingine kwa jinsi ileile; na kwamba hakuna mmoja unaopewa mamlaka ya kuingilia mwingine.

Pia kwamba katika mambo muhimu hakuna mhimili unaofanya mambo yote katika mchakato mzima, bali hufanya sehemu yake na mhimili mwingine kukamilisha yale yaliyosalia.

Mfano mzuri unaoonyesha uhakiki wa uwiano huo ni kama vile bunge linapotunga sheria, lakini Rais wa Tanzania ambaye ni mhimili wa utawala, anaweza kukataa sheria hiyo.

Iwapo ataikubali sheria hiyo na kuipitisha, bado inabaki kwamba ama bunge au utawala hawawezi kusimamia ufafanuzi wa sheria hizo na kutolea hukumu. Wenye mamlaka ya kufanya hayo ni mhimili wa mahakama.

Katika baadhi ya katiba za mataifa, ipo nafasi ya bunge kumpinga rais kwa kura za kutosha pale ambapo amekataa kupitisha sheria iliyotungwa na bunge.

Wakati huohuo mhimili wa utawala wanao wajibu wa kuhakikisha kwamba vyombo vya dola vinao wajibu wa kusimamia ulinzi wa sheria hizo ndani ya mipaka ya taifa husika.

Kwa hiyo, haiwezekani bunge kusimamia utendaji wa majeshi lakini pia siyo sahihi mhimili wa utawala kutumia jeshi kulazimisha bunge kupitisha sheria fulani.

Pale ambapo mhimili mmoja huvuka mipaka na kuingia katika mamlaka ya mhimili mwingine hizo ni dalili za kukiukwa kwa utawala wa demokrasia.

Zimekuwepo kauli tata kwamba wakati mwingine kuwa mhimili wa utawala ndio unaoendesha shughuli za nchi za siku kwa siku; una idara nyeti kama za ukusanyaji wa mapato; usimamizi wa usalama wa watu na mali zao; ulinzi wa taifa; uendeshaji wa wizara mbalimbali; hivyo mhimili huu una mamlaka juu ya mingine. Huu ni uelewa potofu.

Ikumbukwe kwamba uendeshaji wa mambo yote katika taifa hufanyika kwa mujibu wa sheria ambazo hutungwa na bunge na kufafanuliwa na mahakama pale kunapotokea ukwazo.

Hivyo basi, mihimili yote ni sawa na muhimu nyakati zote. Mapato yanayokusanywa na mamlaka zilizo chini ya mhimili wa utawala siyo mali ya mhimili huo, bali ni mali za wananchi walipa kodi kwa ajili ya uendeshaji wa nchi.



**Na Evarist Chahali**
evarist@chahali.com

# Pembe nne za kadhia ya umeme

MAJUZI nilitwiti - "nasikia Tanesco wameshafanya yao huko Arusha" baada ya kufahamishwa na mdau mmoja kuwa shirika hilo la ugavi wa umeme limekata nishati hiyo.

Muda mfupi baadaye, nikapokea mrejesho kutoka zaidi ya mikoa 10 ambayo pia ilikuwa "kizani" kutokana na Tanesco "kuchukua umeme wake."

Tukio hili lilinifanya nijibidiishe kuifahamu historia ya tatizo la kukatika umeme nchini Tanzania. Na haikuchukua muda kukutana na andiko ambalo japo siyo la kitaalamu, lilieleza kwa kina kuhusu suala hilo.

Nanukuu, "Historia inaonesha kwamba mgao usio wa kawaida wa umeme kwa nchi yetu kwa miaka ya karibuni ulianza mwaka 1992, kufuatia ukame wa muda mrefu ambao uliikabili nchi kwa sehemu kubwa, ukizingatia kwamba kwa kipindi hicho, sehemu kubwa ya umeme uliokuwa ukitumika hapa nchini ilitokana na nguvu ya maji (hydropower) na mafuta mazito (Heavy Fuel Oil – HFO)."

Kwa maana hiyo, tatizo hilo limedumu kwa takriban miaka 30 sasa. Hata hivyo, kuna nyakati makali ya kukatika kwa umeme yamekuwa pungufu au zaidi ya vipindi vingine.

Kwa vile katika muda wote huo Tanzania imekuwa chini ya utawala wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), yayumkinika kuhitimisha kuwa tatizo hilo ni miongoni mwa kufeli kwa chama hicho tawala.

Kinachokera zaidi kuhusu tatizo hilo endelevu ni jinsi linavyoshughulikiwa na angalau pande nne muhimu – wanasiasa wa CCM, wanasiasa wa upinzani, Tanesco wenyewe na wananchi kwa ujumla.

Ili kubaini mtazamo wa CCM kuhusu tatizo hilo, jiulize swali hili - "lini umemsikia kiongozi wa ngazi za juu akiongelea 'mgao wa umeme' achilia mbali kutaka ufumbuzi wa tatizo hilo upatikane"? Kwa kifupi, hakuna utashi wa kisiasa miongoni mwao kuhusu utatuzi wa tatizo hilo.



*Mkurugenzi Mkuu Tanesco, Maharage Chande*

Kwa upande wa wanasiasa wa upinzani, ukiachilia mbali malalamiko ya hapa na pale, hawajachukua hatua za makusudi kuibana CCM kuhusu mgao wa umeme. Zi wapi kampeni za kuishinikiza CCM imalize tatizo hilo?

Kuhusu Tanesco, ni wazi kuwa shirikia hilo limeshindwa kazi. Nini kifanyike, wanajua watawala wetu.

Kwa upande wa wananchi, kosa kubwa ni kukubali kuwa mgao wa umeme ni stahili yao.

Mwisho, taarifa kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania zinaonyesha kuwa sasa pia kuna "mgao wa maji" ambao ukichanganya na mgao wa umeme, inakuwa kama nyoka mwenye vichwa viwili.

# Nani mwizi wa laptop 13?

**Na Waandishi WETU**

KOMPYUTA mpakato (Laptop) 13, mali ya baadhi ya abiria zilizokuwamo ndani ya ndege ya Kampuni ya Precision Air iliyopata ajali mjini Bukoba, zimeibwa, Pambazuko linaweza kueleza pasi na shaka.

Ndege ya shirika hilo ililazimika kutua ndani ya maji – Ziwa Victoria, mita chache kutoka Uwanja wa Ndege wa Bukoba, Kagera na kusababisha vifo vya abiria 19, huku abiria wengine 24 wakiokolewa. Ajali hiyo ilitokea Novemba 6, mwaka huu majira ya saa 2.53 asubuhi.

Pambazuko linazo taarifa za uhakika kuwa baadhi ya mizigo ya abiria; walionusurika na wale waliopoteza maisha, ilibebwa na kupelekwa Hospitali ya Mkoa kwa ajili ya huduma za tiba na wengine miili yao kuhifadhiwa baada ya kubainika kufariki dunia.

Mizigo iliyokusanywa kutoka kwenye ndege hiyo ilipelekwa hospitali hapo ni pamoja na mabegi yaliyokuwamo kwenye eneo la abiria (cabin) na mingine iliyokuwa eneo mahsusi kutunza mizigo (luggage compartment).

Pambazuko limewatafuta baadhi ya walionusurika kwenye ajali hiyo na kuwahoji kuhusu usalama wa mizigo yao, na wengi wamekiri kupokea, lakini mingi ikiwa imefunguliwa na kutolewa baadhi ya vitu, hasa vyenye thamani, zikiwamo laptop.

Daktari Felix Otieno amekiri kupata mizigo yake, lakini begi lililokuwamo ndani ya eneo la kuketi abiria, halikuwa na laptop, na kwamba alileteka akiwa hospitali.

"Mimi niliambiwa mizigo yetu imekusanywa mahali hapo hospitali tulipokuwamo, lakini nilipokagua yangu, sikukuta laptop, na sikuwa na muda wa kuuliza maana bado nilikuwa na kiwewe, na hata sasa sijui nani aliichukua," ameliambia Pambazuko jana.

Ofisa mmoja wa Mradi wa Bomba la Mafuta la Tanzania na Uganda (Eacop) ameliambia Pambazuko kuwa mfanyakazi wao mmoja, raia wa Uingereza ambaye alikuwa moja wa marehemu, Jonathan Rose, kwenye mizigo yake kulikosekana laptop.

"Jon alikuwa na laptop, na kwa kazi zake, ni lazima kuwa na kifaa hicho kwa ajili ya kazi, lakini begi lake halikuwa na laptop, na hata wakati linachukuliwa pale hospitali, lilionekana kufunguliwa," anaongeza huku akikataa kutajwa jina gazetini.

Ndugu wa Aneth Kaaya, binti aliyekuwa akielekea Bukoba kujitambulisha ukweni, inaelezwa na ndugu zake kwamba hakuwahi kusafiri bila laptop, lakini wakati wanakabidhiwa mizigo ya ndugu yao, hawakuona laptop yake.

Mwingine ambaye laptop yake haikuonekana ni manusura Eva Mcharo, mtumishi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru). Huyu anaeleza kuwa mizigo yake ilikutwa imefunguliwa na hakukuwa na laptop.

Wengine ni watumishi watano wa Menejimenti na Maendeleo ya Afya (MDH), waliokuwa wakifanya kazi makao makuu, Dar es Salaam; hawa inaelezwa kuwa wote walikuwa na laptop, lakini kwenye mizigo iliyokusanywa na kukabidhiwa, hakukuwamo vifaa hivyo muhimu kwa ajili ya kazi.

Wafanyakazi wote hawa walifariki dunia ambao ni pamoja na watafiti watatu wakiwemo Dkt. Boniface Jullu, Dkt. Neema Faraja na Dkt. Alice Simwinga pamoja na Sauli Happymark pamoja na mkuu wa kitengo cha mawasiliano, Zarcharia Mlacha.

*Inaendelea Uk. 14*

# Maji kuibua mgogoro

**Na Mwandishi WETU**

KUENDELEA kuwepo kwa uhaba wa maji katika maeneo mengi ya Tanzania, kunatishia kuitumbukiza nchi katika mgogoro wa usalama wa kijamii endapo hatua za haraka hazitachukuliwa na serikali.

Uhaba huo umetokana na mabadiliko ya tabianchi yaliyoikumba nchi kwa miaka miwili mfululizo sasa, na hivyo kushusha kina cha maji katika mito mikubwa ambayo inabeba vyanzo vya maji. Mito hiyo ni pamoja na Mto Ruvu, Mto Pangani, Mto Rufiji, na mito mingine nchini nzima.

Tatizo la ukosaefu wa maji limekuwa sugu maeneo mengi ya Tanzania, lakini sasa limeonekana kuwa kubwa baada ya kadhia hiyo kulikumba Jiji la Dar es Salaam.

Pambazuko linatambua kuwa hivi sasa jiji hilo lenye wakazi wanaoweza kufikia milioni 6, linapata maji pungufu ya kiwango chake. Jiji hilo linapaswa kupokea maji lita milioni 466 kwa siku, ingawa sasa linapokea lita milioni 300 tu.

Ikiwa hali hii itaendelea, kuna uwezekano usalama wa afya za wananchi, hasa wa majiji makubwa, kukumbwa na mlipuko wa magonjwa yanayotokana na kutokuwepo kabisa kwa maji au kutumika yale machafu.

Magonjwa haya ni pamoja na kuwepo mlipuko wa kipundupindu, kuhara, magonjwa ya ngozi na kuharibika kwa mfumo wa upumuaji.

Khamis Kamese, daktari katika polikliniki ya Kasese, Magomeni, Dar es Salaam, anasema kuwa kukosekana kwa maji ama kutumika kwa maji machafu, ni hatari zaidi kwa ustawi wa binadamu.

Anasema, serikali inapaswa kuchukulia kukosekana kwa maji kama vita, kwamba inapaswa "kupigana kwa silaha zote ili



*Maji ya to Ruvu*

kuhakikisha maji yanapatikana."

Upungufu wa maji katika Mto Ruvu umesababisha mgao mkali wa maji umelikumba jiji la Dar es Salaa, na miji mingine nchini, kufuatia tatizo la mvua duni lililoikumba Tanzania kwa miaka miwili sasa.

Kwa sababu hii, tayari serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Dar es Salaam (DAWASA), wametangaza ratiba ya mgao wa maji kwa wakazi milioni sita wa jiji hili, ambapo, wananchi watapata maji kwa zamu zinazopishana kwa siku moja moja.

Serikali inasema kuwa utaratibu huu utaendelea hadi hapo mabadiliko ya hali ya hewa yatakapokuwa rafiki kwa mahitaji ya maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ameliambia Pambazuko kwamba mgawo wa maji utaendelea hadi hapo kutakapopatikana uhakika wa maji kutoka maeneo mengine, lakini siyo kutegemea Mto Ruvu pekee.

"Kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi, maeneo mengi nchini yalipata mvua duni msimu uliopita, kwa msimu huu wa sasa, mvua zimechelewa, na

*Inaendelea Uk. 12*

# Maji kuibua mgogoro

jambo hili liko nje ya uwezo wa serikali," ameongeza Makalla.

Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kuwa, uhaba wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani hapa nchini Tanzania ni tatizo ambalo halipaswi kuwepo.

Kwa mujibu wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji iliyosomwa bungeni na waziri wake, Jumaa Hamidu Aweso, Mei 2022, "rasilimali za maji zilizopo nchini zinakadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka; rasilimali za maji juu ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 105 na zilizopo ardhini ni mita za ujazo bilioni 21.

Alisema kuwa, hadi kufikia Aprili 2022, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini yalikadiriwa kuwa ni takribani mita za ujazo bilioni 47 kwa mwaka sawa na asilimia 37.37 ya maji yaliyopo nchini.

Aweso aliliambia Bunge kwamba, mahitaji hayo ya maji nchini yanatarajiwa kuongezeka hadi kufikia wastani wa mita za ujazo bilioni 80 kwa mwaka ifikapo mwaka 2035.

Lakini, akasisitiza kuwa, kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa mita za ujazo 2,250 kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu milioni 55.9 kwa mwaka 2019.

Kimataifa, kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka ni wastani wa mita za ujazo 1,700. Chini ya hapo nchi inahesabika kuwa na tatizo la uhaba wa maji, yaani "water stress." Kwa hiyo, nje ya changamoto ya ukame, Tanzania hatuna tatizo la "water stress."

Hata hivyo, athari za mabadiliko ya tabianchi zimeendelea kuathiri sekta ya maji kwa kusababisha kukauka kwa vyanzo vya maji, kuongezeka kwa migao ya maji pamoja na kuharibika kwa miundombinu ya maji.

Waziri Awezo ameliambia Pambazuko kwamba katika kukabiliana na changamoto ya tabianchi, serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali, ikiwamo kuboresha huduma ya maji katika miji 28, Tanzania Bara na Zanzibar kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 500.

Amesema kuna miradi ya kuvuta maji kutoka kwenye maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa na kuyasogeza kwenye vijiji vya wananchi.

Mkakati mwingine wa serikali ni kujenga mabwawa 174 makubwa ya kimkakati ili kuyasogeza maji karibu na wananchi kwenye mikoa yenye ukata mkubwa wa vyanzi vya maji.

Hata hivyo, Pambazuko limeshindwa kupewa majibu ni nini serikali inafanya kuhakikisha kuwa inaanza kujenga mfumo wa maji ya akiba katika mtazamo wa kitaifa.

Kiongozi mmoja wa juu wa serikali katika wizara ya maji, alipobanwa kuhusu hili alisema aulizwe waziri, lakini baadaye akarejea kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi ya simu akieleza kuwa serikali imeanza kusaka njia bora ya kuwa na akiba kubwa ya maji kwa kila wilaya.

Hata hivyo, kama alivyogoma kutajwa jina lake gazetini, ndivyo hivyhivyo, alivyokataa kueleza njia hizo alizoziita bora za kutunza maji kwa wingi.

Pambazuko linaweza kueleza pasipo shaka kuwa Tanzania inahitaji visima vya maji ya akiba 68,647 (ikiwa ni jumla ya vitongoji 64,384 na mitaa 4,263), kila kimoja kikiwa na ujazo wa wastani wa meta 1000, sawa na urefu wa meta 10, upana wa meta 10, na kimo cha mita 10.

Kuna njia nyingi za kutafuta fedha hizi, zikiwemo kukata matumizi ya serikali yasiyo ya lazima. Lakini, huenda juhudu hizi zisikidhi mahitaji yaliyopo kwa ajili ya kujenga mfumo wa maji ya akiba kwa taifa zima, tena katika utaratibu wa dharura.

# Wazazi watenge muda mrefu wa kulea

**Na Tryruckia MFINANGA**

UHAKIKA ni kwamba maisha ya sasa yamebadilika sana, familia nzima kila kunapokucha – inahama nyumbani na kwenda maeneo mengine kwa ajili ya kutimiza mzunguko wa siku.

Katika maeneo ya mijini, wapo wanaoenda kazini; hasa baba na mama na wapo wanaoenda shuleni; hawa ni wale watoto wenye umri wa kwenda shule, iwe shule za awali (chekechea), shule za msingi na hata sekondari.

Zamani, maisha yalikuwa tofauti kidogo, aliyekuwa akienda kazini, alikuwa ni baba wa familia; haijalishi kazi gani, ilimuradi anadamka na kwenda kwenye kibarua chake, lakini sasa maisha yanalazimisha kila mwenye umri wa kufanya kazi anafanya.


Baba atadamka na mama wa familia vivyo hivyo na wote wanawahi vibaruani, huku watoto nao wakiwahi shuleni.

Wanaobaki nyumbani ni wasaidizi ambao kazi yao kubwa ni kulea watoto wadogo; kuwapikia, kuwalisha, kuwaosha na kuwapa huduma zote zinazostahiki wakati mama (na hata baba) wa familia hayupo. Pia wasaidizi hawa wa nyumbani ndiyo wanaofanya usafi na kuwa walinzi wa mali.

Kutokana na mpangilio wa maisha ya sasa, wazazi hawana muda wa kukaa na kuwatambua watoto wao; wengi wamebaki kuamini kuwa kazi kubwa ya malezi ya watoto ni kuwaletea vyakula, vinywaji na kulipa ada.

Hakuna mzazi mwenye muda mwingi wa kufuatilia mwenendo wa maisha ya watoto wake. Baba na mama wote wako "bize" wakihangaika kusaka pesa za mahitaji na kamwe siyo kusaka muda wa kuwajengea tabia njema kwa watoto wao.

Ni kutokana na tabia hii, watoto wengi-




wa kike na kiume, wamekengeuka. Wamekuwa na tabia mbaya zisizomithilika, na wazazi wanakuja kutambua hilo tayari mtoto ameshakuwa sugu na kuharibika zaidi.

Katika maisha ya sasa sio jambo la ajabu kuona wazazi kwa wiki nzima hawana muda wa kukaa na watoto wao hata kwa saa mbilii na kuona maendeleo ya vijana wao ya kitaaluma na kitabia pia kutokana na harakati za maisha.

Familia nyingi zimekuwa chini ya malezi yasiyokuwa ya wazazi zaidi ya yale ya wasaidizi wa nyumbani, ambao nao hawana muda zaidi ya kulea kwani wako 'bize' pia na kufuatilia tamthilia kwenye televisheni.

Ni kutokana na 'ubize' wa wazazi na kushindwa kuwafuatilia watoto wao, vijana wengi wakiwa na umri mdogo wamejenga tabia mbaya ambazo zimekuwa zikiongezeka kwa kasi kubwa kila uchao katika Tanzania.

Siku hizi, habari za magazetini, redioni na televisheni, haziwezi kupita bila kuwepo habari za watoto kubakwa, kulawitiwa na kufunzwa matumizi ya dawa za kulevya. Haya ni matokeo ya watoto kutokuwa na muda wa kuzungumza na kusimamia vyema mienendo ya watoto wao.

# Nani mwizi wa laptop 13?

Watumishi wa MDH ambao ni manusura na kwamba nao walipoteza laptop zao ni Nickson Jackson, Dkt. Josephine Mwakisambwe na Dkt. Felix Otieno.

Manusura mwingine, Emil Mwesiga anashangaa iweje watu wahangaike na laptop ambazo huenda hata zisifanye kazi kwani nyingi zitakuwa zililowa maji.

"Nashangaa binadamu sijui tumekuwaje, watu wanahangaika kuiba mali za watu waliopata ajali, na sijui zinawasaidia nini, ni ajabu sana," anaongeza huku akionekana kukwerwa na tabia hiyo.

Pambazuko ambalo liliwahi kufika eneo la tukio muda mfupi baada ya ndege hiyo kutua majini, halikuona waokozi wakihangaika na mizigo na hata manusura hawakutoka na mizigo, hivyo mingi ilibaki ndani ya ndege.

Juhudi za kupata uthibitisho wa nani alimuru mizigo hiyo itolewe bila kuwepo usalama wa uhakika na ipelekwe hospitali badala ya kuhifadhiwa mahali pengine, ziligonga mwamba baada ya uongozi wa uwanja wa ndege wa Bukoba kusema upewe muda kufuatilia.

Kumekuwepo mazoea ya baadhi ya wananchi kugeuza ajali za magari, hasa ya abiria kuwa "chumio" kwa kuiba mali za manusura na hata wanaofariki dunia.

Pambazuko

**Gazeti la Pambazuko sasa limeanza kupokea matangazo**

Ewe mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali ipaka ya neo ulilopo, tangaza nasi kwa kuwasiliana kupitia namba hii: 0744 768 263 au Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

***Karibu sana Pambazuko isaidie kuipaisha na kuipambazua biashara yako.***

# Haki inapobakwa mchana kweupe

**Na Godlisten MALISA**

KATALA Kikaja na Ng'hulima Lilanga walikuwa mawakala wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kwenye uchaguzi mkuu 2020, kata ya Dutwa, Wilaya Bariadi mkoani Simiyu.

Usiku wa Oktoba 27, 2020 walipewa vitisho na viongozi wa chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwamba wasiende kusimamia kura za wagombea wa Chadema kwa sababu hasa walitaka kuhakikisha kuwa mgombea wa urais kwa tiketi ya CCN, John Magufuli anapata ushindi wa asilimia 100 katika eneo lao.

Wanachama hawa wa Chadema, wakapuuza vitisho hivyo. Oktoba 28, 2020 – siku ya kupiga kura, waliwahi vituoni alfajiri, mmoja akisimamia Dutwa A na mwingine Dutwa B. Wakiwa hapo walisikia taarifa kuwa kuna mawakala wamezuiwa kuingia vituoni na wengine wameingia, lakini wakatolewa kwa nguvu na polisi.

Lakini wao wakaendelea kubaki vituoni, wakisubiri zoezi la kupiga kura lianze. Ghafla wakaja polisi wenye silaha ambao walitumia nguvu kuwatoa na kuwafunga pingu. Wakapelekwa kituoni bila kuwaeleza kosa lao. Uchaguzi ukamalizika na matokeo yakatangazwa wakiwa bado rumande.

Mwezi mmoja baadaye wakapandishwa kizimbani kwa tuhuma za ubakaji na unyang'anyi wa kutumia silaha. Wakastaaajabu sana. Wakajiuliza wamembaka nani? Lini na wapi?

Hati ya mashtaka ikaeleza kuwa alfajiri ya Oktoba 28, 2020 walipoenda kituo cha kupiga kura, walimkuta msimamizi msaidizi wa uchaguzi, ambaye walimbaka kwa zamu, kisha wakampora pesa taslimu Sh. 300,000. Baada ya kufanya tukio hilo, wakabaki kama mawakala wa Chadema wakisubiri kusimamia kura.

Jambo la ajabu hati ya mashtaka



*Katala akiwa na Nghulima*

haikumtaja huyo aliyebakwa wala hakuitwa mahakamani kutoa ushahidi. Aliwasilisha ushahidi wake kwa maandishi kwa kile kilichoelezwa kwamba ni kumlindia utu wake. Mahakama ya Hakimu Mkazi Bariadi ikawahukumu kifungo cha maisha jela.

Baada ya kusota jela kwa miaka miwili, wakakata rufaa. Hatimaye wiki iliyopita, Mahakama Kuu - Kanda ya Shinyanga imewaachia huru. Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Athuman Matuma amesema ushahidi uliowatia hatiani ulikuwa "dhaifu, unaotia shaka na usiokubalika kisheria."

Miaka miwili ya mateso, miaka miwili ya kupakaziwa kesi, miaka miwili ya kutumikia adhabu bila hatia. Kama siyo kukata rufaa, vijana hawa wangemalizia maisha yao yote gerezani na kuacha familia zao zikiteseka.

Na dunia nzima ingewahukumu kama majambazi na wabakaji maana mahakama iliwahukumu hivyo.

# Uhalifu unaodhibitiwa kihalifu

**Na Jabir IDRISSA,**
**Zanzibar**

KWENYE mitaa na vichochoro maeneo ya ng'ambo ya mji wa Zanzibar, hususan katika wilaya za Magharibi A na B, utakuta picha mbili zikisawiri.

Moja ni ya gubiko la simulizi kuhusu vitendo vya vijana machachari ambao ni kama wameshindikana kimalezi kwenye himaya za familia zao. Hawa vijana kwa sehemu kubwa kutoka familia maskini, ni 'choka-mbaya' na 'waliopigika' na sasa wanasaka tonge kibabe.

Ni vijana fukara, baadhi wakiwa wanaonekana kuwa na afya mbovu kutokana na kuathirika na kutumia dawa za kulevya kwa jina maarufu "unga." Wenzao kama wao, wamepigika kwa bangi wanayovuta kwa ajili ya kupitisha muda huku wakitamani kusafiri kwenda ughaibuni pasina viza.

Kati yao, wapo waliomaliza elimu ya sekondari na kutosonga kutinga chuo kikuu. Hawana wanalojua au hohehahe kwa sababu fursa ya ajira rasmi - serikalini au sekta binafsi, imewapita upande na ile ya kujiajiri 'haijatiki' kutokana na ukosefu wa mtaji na 'konekshen.' Hawa njaa-njaa kabisa.



*Mazombi*

Lakini baadhi yao wanatoka familia zinazojielewa ila imeshindikana kuwasaidia ili kujenga misingi ya maisha ya kujitegemea.

Hawa vijana walikuwa wachache zaidi, lakini hivi sasa wameongezeka na kutishia amani ya wananchi wakiwemo wanafamilia zao kwa kupora mali zao kuanzia simu za mkononi, pochi mpaka chochote wakipatacho.

Hawa hupora baada ya kukunjia makucha wananchi na kuwatishia kwa mapanga na visu. Vijana wanataka fedha na mali. Wanapigania maisha ya ujana wao baada ya kukata tamaa ya msaada.

Hawa eti wamepewa jina la pakarodi na paka-vichochoro - mfano wa wale panya-rodi wa mitaani jijini Dar es Salaam.

Picha ya pili ni kundi la "majitu" waliovalia nguo zisizo sare rasmi. Wanapanda gari ziso nambari- sajiliwa wakiwa wamejazana kwenye LandRover (Defender), huku baadhi yao wamefunika nyuso zao. Wameshika silaha za moto ila wachache wakishika bunduki na wengine marungu na mapande ya nondo huku wakiranda barabara za mitaani "bukheri wa afya."

Baada ya ongezeko la wale panya-mitaa kukithiri na kuwa vijana watukutu, palisikika sauti za maumivu makali kutokana na vijana hawa kujipanga magenge na kuvamia wananchi usiku na mchana na kuwaibia simu na mali zao nyenginezo.

Hupita kwenye vijia vya ndani kidogo ya njia kuu na kushtukiza watu - wawili au zaidi walioketi - walio mapumzikoni baada ya pirika za mchana kutwa.

Kwa hivyo picha hizi mbili ni za watu wanaoviziana. Hawa wanatafuta kuganga njaa kwa njia haramu - uhalifu - huku

*Endelea Uk. 17*

# Uhalifu unaodhibitiwa kihalifu

wale wakitaka kuwadhibiti.

Hawa ambao tungeita askari wema, hawapo rasmi kwamba hakuna anayeweza kuwatambua kuwa huyu ni askari fulani. Wanatambuliwaje askari wa serikali? Mavazi yao; iwe Jeshi la Ulinzi, Polisi au hata wale vikosi mahsusi vya Zanzibar.

Uhakika ni kwamba wanazo sare zao rasmi, lakini hawazivai, wanavaa mararu na kujifunika nyuso kwa kutumia vitambaa vinayotisha kama si soksi. Kwa kuwatambua ni askari wa serikali ni mazoea kuwaita majina tofauti ikiwemo Janjaweed na Mazombi.

Huu mfumo wa mavazi mararu wanayovaa, kutumia gari zisizo namba zilizosajiliwa na kuwa wamebeba silaha za jadi huku wameziba nyuso zao kwa matambara yasoeleweka, unatosha kuwachukulia kama wahalifu wengine.

Iweje askari wa serikali wafiche utambulisho wao wakati kila kikosi - vile vilivyo chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar - kina vazi lake rasmi?

Inaeleweka kuwa kundi hili la 'askari' ndilo linalotumika kiharamia kuvuruga uchaguzi Zanzibar kwa maelekezo ya wakubwa na lengo likiwa kukidhi matakwa ya kisiasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Sasa katika mfumo uleule wa mashambulizi yao kwa wananchi wakati wa uchaguzi - kushughulika na waliomo na wasiokuwemo, ndivyo wanafanya katika kudhibiti wahalifu. Kwa hakika huu wao ni uhalifu unaotumika kudhibiti uhalifu. Kivipi sasa?

Kufikia wiki hii vijana 150 wamefikiwa na kushambuliwa kwa jina la wahalifu. Wamepigwa ikiwemo maeneo ya viungo vyao, na kuvunjwa vidole na vingine kukatwa.

Maahambulizi hufanywa usiku kwa kufuatwa majumbani mwao, wakichukuliwa katika namna ambayo mtu unaamini kuna orodha imeandaliwa kabla. Na ufuatiliaji unathibitisha ofisi za masheha zimetumika kubainisha wanaoitwa "vijana wahalifu."

Nimesimuliwa maguvu ya askari wasojitambulisha wala kujulikana nani ni nani, inaumiza na kukera.

Kijana mmoja katika moja ya maeneo ya Unguja alikutwa dukani kwake kiasi cha saa 5 usiku, akiwa pamoja na watu wengine wawili ambao waliamriwa kufunga biashara na kuambiwa wajifungie ndani ya duka.

Waliotoa amri hiyo haramu ni Mazombi waliofika hapo kwa gari aina ya Defender wakiwa wamejazana na gari jingine dogo – waliwafungia vijana hao kwa zaidi ya saa moja huku wakisikika kutoa vitisho vya kuwadhulu.

Hatua hii inashangaza sana, vijana wanatafuta mkate wa familia halafu wanafungiwa ndani na vyombo vya serikali ambavyo vinapaswa kuwa mstari wa mbele kulinda na kamwe siyo kutesa.

Kwenye nchi huru inayosifiwa kuwa kisiwa cha amani na ambayo uongozi wa serikali umejipambanua kuwa wa maendeleo kupitia kaulimbiu ya uchumi wa bluu, unaaminije kila kitu kiko sawa kwa staili hii ya kupambana na uhalifu?

Uhalifu unakomeshwa kwa kuwatenga Jeshi la Polisi lenye wajibu wa kisheria kulinda usalama wa raia na mali zao ingawa hizi hatua za kutumia "askari wasojulikana" zimekuja kuvuruga, kuonea na kuharibu.

Uhalifu unakera. Unaumiza miili na unatia umaskini. Wananchi wangetamani kuona unakomeshwa kwa utaratibu wa kisheria wa kuchukua waliohusika nao badala ya kufyeka aliyemo na asiyekuwemo.

Hofu ya wengi ni kuwa operesheni ya Mazombi inajenga chuki pale inaposhika na kuwatia ulemavu vijana wasiohusika - na pengine waliotajwa kwenye orodha zilizoandaliwa kisiasa na Masheha - huku kukiwa hakuna fidia yoyote kwa walioonewa.

Inakuwa hatari zaidi endapo mfumo huu wa kihalifu unatumika kudhibiti uhalifu mdogo, tena ukiwa umepata baraka za uongozi wa juu wa serikali.

# Asili ya Banyamulenge wa Kitutsi DRC

**Na Mwandishi WETU**

BANYAMULENGE ni jamii ya Watutsi wanaoishi eneo la Mlima Mulenge, iliyoko Wilaya ya Uvira, Jimbo ka Kivu Kusini, Mashariki mwa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Kiutamaduni jamii hii haina tofauti yoyote na kabila la Watutsi wa Rwanda na Burundi.

Banyamulenge walichagua jina hili miaka ya 1970 ili kuepuka kuitwa "Wanyarwanda" na kuonekana kama wageni au wahamiaji.

Hawa huzungumza Kinyamulenge, lugha ambayo ni mchanganyiko wa Kinyarwanda na Kirundi, ingawa inatofautiana katika fonolojia na mofolojia kadhaa.

Banyamulenge ni kabila lililopata umaarufu kwenye maasi ya "Operation Banyamlenge." Maasi haya ndio yalisababisha vita ya kwanza ya Kongo ya mwaka 1996-1997 na ile ya pili ya mwaka 1998-2003.

Kihistoria, Banyamulenge walihamia DRC kwenye karne ya 17 wakitokea Rwanda na Burundi.

Kikundi cha Kwanza cha Wanyarwanda kuhamia Kivu Kusini ni kile kilichofika eneo hilo la Mulenge na kuweka makazi yao mwaka 1850. Kikundi cha pili kilifika mwaka 1880,

Sababu za kuhamia huko ni kutokana na kutofautiana na Mwami Rwabugiri wa Ufalme wa Rwanda juu ya ushuru uliowekwa kuwataka kulipia mifugo yao.

Kikundi cha tatu ni Watutsi waliokimbia vita vikali vya urithi vilivyoibuka mwaka 1895 baada ya kifo cha Rwabugiri.

Kikundi hiki kilikuwa na Watutsi na Wahutu jamii ya Abagaragu, ambao walikuwa wamekataa mvutano wa kikabila, hivyo wakaamua kuhama na kutafuta makazi mapya. Hawa walihamia eneo la Bonde la Ruzizi kwenye Uwanda wa Itombwe.

Uwanda huu una urefu wa mita 3000 kutoka usawa wa bahari, na haufai kwa kilimo, lakini unafaa kwa malisho ya ng'ombe, hivyo wakaweka makazi hapo.



***Rais Kayibanda***

Kikundi cha nne, ni kile kilichopo eneo la Luberizi. Hawa ni Watutsi jamii ya "Wanyakarama" waliokuwa chini ya Ufalme wa Burundi chini ya Mwami Rusizi, Ila mipaka ya wakoloni iliyowekwa mwaka 1899, iliwaweka hawa watutsi ndani ya Kongo DRC.

Hivyo eneo hili la Luberizi lipo Jimbo la Kivu Kusini na hawa banyamulenge wa Nyakarama wanaozungumza Kirundi.

Kikundi cha tano, ni kile kilichopo Jimbo la Ituri, hawa hufahamika kama Wahima sawa na Wahima wa Uganda ambao huzungumza lugha moja na Wanyankole/Watoro wa Uganda. Hawa waligawanywa na mpaka ulio wekwa mwaka 1884 baina ya Waingereza na Ubelgiji.

Wahamiaji wengine wa Kinyarwanda waliendelea kuhama na kuwasili Kongo Mashariki kuanzia miaka ya 1925 hadi 1929. Kuanzia miaka ya 1930, wahamiaji wa Rwanda waliendelea kuhamia Kongo kutafuta kazi na malisho ya mifugo yao.

Idadi kubwa ya wahamiaji wa Kitutsi ilishuhudiwa mwaka 1959-1960 kufuatia "Mapinduzi na Uhuru wa Rwanda" yaliyoongozwa na Wahutu wengi chini ya chama cha Pelpe Hutu chini ya Grégoire Kayibanda aliyekuja kuwa Rais wa Rwanda.

*Itaendelea*




# Viambishi vya upatanisho wa kisarufi

**Na Dkt. Michael Mashauri**

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo tutakuwa na darasa juu ya viambishi vya upatanisho wa kisarufi (Noun class agreement (Subject concord).

Kila ngeli ina viambishi vyake vya upatanisho wa kisarufi. Viambishi hivyo hujitokeza katika vioneshi, vivumishi na vitenzi.

Kila nomino iko katika ngeli fulani na huwa na kiambishi chake cha upatanisho katika sentensi. (Each noun class has its subject concord. These prefixes feature in demonstratives, adjectives and verbs. Every noun is under a certain noun class and it has its noun class agreement prefix in the sentence.) Examples:

| Noun Class | EXAMPLES | |
|---|---|---|
| M/WA | Singular | 1st - Mimi **ni**likula wali jana (I ate rice yesterday)<br>2nd - Wewe **u**tapika (You will cook)<br>3rd - Yeye **a**takuja (He/she will come) |
| | Plural | 1st - Sisi **tu**lilala jana (We slept yesterday)<br>2nd - Nyinyi **m**nakula ugali (You are eating ugali)<br>3rd Wao **wa**tacheza mpira wa miguu (They will play football) |
| M/MI | Singular | Mguu **u**mevunjika (A leg is broken) |
| | Plural | Miguu **i**mevunjika (Legs are broken) |
| JI/MA | Singular | Nanasi **li**napendeza (A pineapple is looking good) |
| | Plural | Mananasi **ya**napendeza (Pineapples are looking good) |
| KI/VI | Singular | Kiti **ki**metengenezwa na Neema (A chair is made by Neema ) |
| | Plural | Viti **vi**metengenezwa na Neema (Chairs are made by Neema) |
| N/N | Singular | Nguo **i**mechanika (A dress is torn) |
| | Plural | Nguo **zi**mechanika (Dresses are torn) |
| U/N | Singular | Uzi **u**metumika (A thread has been used) |
| | Plural | Nyuzi **zi**metumika zote (All threads have been used) |
| U/MA | Singular | Ugonjwa **u**melipuka (A disease has erupted) |
| | Plural | Magonjwa **ya**melipuka (Diseases have erupted) |
| KU | Singular | Kusoma **ku**navutia sana (Reading is so much attracting) |
| PA-MU-KU | PA- | Pahali **pa**napendeza (The place is looking good) |
| | MU- | Muhali **mu**navutia watu (Inside there attracts people) |
| | KU- | Kule **ku**navutia (That place (there) is attracting) |

Masomo ya vivumishi na vioneshi yataonesha jinsi viambishi hivi vinavyojitokeza katika maneno hayo. (The lessons on adjectives and demonstratives will show how these prefixes feature in those words).

***• Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.***

# Hoja ya kupinga uwepo wa Mungu

**Na Bruno Marcelo**

WAKANAMUNGU ni watu wanaodai haki ya kutoabudu “Mungu” kwa sababu wanapinga uwepo wake.

Baadhi ya hoja zao, bila kuzihakiki, ama zinaanzia kwenye mikanganyiko iliyoko kwenye sifa za Mungu, au kwenye mikanganyiko iliyoko kati ya sifa zake Mungu na sifa za ulimwengu aliouumba yeye, na ni kama ifuatavyo:

Hoja ya kwanza inatiririka kuwa; Kama kungekuwa na Mungu anayejua kila kitu, mwenye upendo usio na ukomo, na mwenye uwezo wa kufanya kila kitu, basi angezuia mateso yaliyoko duniani, kama vile kifo, majanga ya asili, na magonjwa. Lakini, kuna mateso ya aina hii ulimwenguni. Kwa hiyo, hakuna Mungu mwenye sifa hizo kwa mpigo.

Hoja ya pili inatiririka kuwa; Kanuni inayopinga mkanganyiko wa kimantiki inasema kuwa kitu kimoja hakiwezi kuwa na sifa fulani na kisiwe na sifa hiyo wakati uleule na katika mazingira yaleyale; lakini, dini tofauti zinataja sifa za Mungu zinazogongana; kwa hiyo, hakuna Mungu mmoja mwenye sifa zinazofahamika na kukubalika kwa waumini dini zote.

Hoja ya tatu inatiririka kuwa; Kama Mungu yupo, basi habadiliki na ndiye aliumba ulimwengu wote; dhamira ya kuumba ulimwengu inakuwepo, kisha inakoma baada ya tendo la uumbaji, na haya ni mabadiliko; kwa hiyo, Mungu aliyeumba ulimwengu alibadilika kifikra baada ya kuumba ulimwengu; Hivyo, Mungu asiyebadilika na aliyeumba ulimwengu hayupo.

Hoja ya nne inatiririka kuwa; Kama Mungu yupo, basi habadiliki na anajua kila kitu kuhusu jana, leo na kesho; lakini, ukweli kuhusu ulimwengu wa jana, ulimwemgu wa leo, na ulimwengu wa kesho hubadilika kadiri muda unavyobadilika, kama ambavyo uzito wako, kwa mfano, unavyobadilika siku hadi siku; Kwa hiyo, Mungu anajua ukweli tofauti katika nyakati tofauti,


*Mbingu*

na hivyo, anabadilika kifikra; Kwa hiyo, Mungu asiyebadilika ana anayejua kila kitu, hayupo.

Hoja ya tano inatiririka kuwa; Kama Mungu yupo, basi yuko nje ya ulimwengu wa majira na mahali na yuko sehemu zote ndani ya ulimwengu; tangu mwanzo wa ulimwengu Mungu alikuwa na yuko nje ya ulimwengu wa majira na mahali na siyo ndani ya ulimwengu huo, ambako tayari kuna vitu vimeshika nafasi zake zenye ujazo maalum; kwa hiyo, Mungu aliye ndani na nje ya ulimwengu wa majira na mahali, hayupo.

Hoja ya sita inatiririka kuwa; Kama Mungu yupo, basi ni hakimu wa haki na ni hakimu mwenye huruma; hakimu wa haki hutoa adhabu inayoendana na uzito wa kosa, na hakimu mwenye huruma hutoa adhabu ndogo kuliko uzito wa kosa; kwa hiyo, Mungu mwenye sifa hizi mbili hayupo.

***Mwandishi ni mwanafalsafa anayependa kuwepo kwa mjadala kuhusu hoja hii. Pambazuko halina upande katika makala zake.***

# Katiba, sura za ujamaa na ubepari

**Na Deusdedith KAHANGWA**

NI kanuni gani inapaswa kuongoza katika kujenga muundo wa uongozi wa nchi utakaomwezesha kila mdau kuishi kwa amani, uhakika wa kunufaika na haki zake bila hofu.

Hofu kwamba, kwa sababu ya madaraka yake makubwa, serikali itafanya jeuri ya kuzipokonywa haki hizo, kama wafanyavyo wajamaa, au kuwatelekeza raia wanyonge kama wafanyavyo mabepari?

Jawabu muafaka linatoka kwa mwanafalsafa na mwandishi wa Kiitaliano, Raffaele Luigi Pecci (1810-1903) – kupitia kitabu chake kimoja kinaitwa, "Kiu ya Mabadiliko ya Kimapinduzi," yaani "Rerum Novarum" kwa Kilatini, kilichochapishwa mwaka 1891.

Kwa mujibu wa Pecci, "sera ya ujamaa na kujitegemea," yaani "the principle of subsidiarity," ndio njia bora zaidi ya kujenga jamii moja ya watu walio sawa na huru dhidi ya mabaya ya ujamaa na ubepari.

Sera hii inaweza kutetewa kwa kutumia ushahidi ufuatao kutoka kwenye muundo wa uongozi wa nchi:

Kwa sababu ya hulka yake, kila binadamu anayo haki ya kushirikiana na wenzake kuunda "jumuia" mbalimbali kwa ajili ya kuzitumia kama majukwaa ya kufanikisha mahitaji yasiyoweza kupatikana nje ya jumuia hizo. Kwa hapa Tanzania, jumuia hizo ni familia, kijiji, kata, tarafa, wilaya, mkoa, na taifa.

Piramidi la jumuia hizi huzaliwa kutokana na ukweli kwamba, kadiri siku zinavyopita, na idadi ya watu kuongezeka katika ngazi moja, ngazi hiyo hushindwa kutosheleza mahitaji mapya, kama vile huduma za shule, soko, mahakama, mgambo na zahanati.

Mahitaji haya huzalishwa kwa kuunganisha jumuia kadhaa za ngazi moja na kuunda "jumuia" moja katika ngazi ya juu, kila ngazi ikiwa na uongozi wake.


*Pecci*

Hivyo, kwa kutumia misamiati chanya, hitimisho ni kwamba, mamlaka ya ngazi ya juu inalo "jukumu chanya" la kuingilia kati, kwa kutoa msaada, kwa watu wa ngazi ya chini, endapo watu hawa, katika upekee wao, hawana uwezo wa kutatua matatizo yao kwa kasi na ukamilifu.

Hivyo, kwa mujibu wa Pecci, kama ambavyo ni kosa kuwapokonya watu binafsi majukumu wanayoweza kuyatekeleza vizuri na kuyaweka mikononi mwa jumuia; vivyo hivyo, ni uvurugaji wa mpangilio muafaka wa "viungo vya mwili" wa jamii, kuyapokonya majukumu yanayoweza kutekelezwa vizuri na jumuia ndogo na kuyaweka mikononi mwa jumuia kubwa.

Pamoja na kanuni hii kutumika katika kuratibu uhusiano uliopo kati ya ngazi tofauti za kiserikali, pia inapaswa kutumika kuratibu uhusiano uliopo ndani ya ngazi tofauti za taasisi, na pia ngazi tofauti za sekta mbalimbali.

Pia inapaswa kutumika kuratibu uhusiano uliopo kati ya dola na mtu binafsi, dola na familia, dola na dini, dola na azaki, dola na sekta binafsi, dola na jumuia ya kimataifa.

# RC wapinga DRC kumegwa

**Na Mwandishi WETU,**

BARAZA la Maaskofu Kanisa Katoliki wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) limepinga juhudi za kijeshi zinazofanywa na nchi za Rwanda na Uganda, kupitia vurugu za waasi wa M23, kwa ajili ya kuigawa nchi hiyo na kuunda taifa jipya liitwalo "North Kivu State."

Katika kikao cha baraza hilo; The Congolese National Episcopal Conference (Cenco), kilichomalizika November 9, 2022, mjini Kinshasa, maaskofu hao, wakiwa wanasukumwa na "jukumu lao la kinabii," walitaka taifa zima kufanya juhudi za pamoja kulinda nchi yao dhidi ya uvamizi wa Rwanda na Uganda.

Waraka wao wa kichungaji wenye kurasa nne, unabeba kichwa cha maneno, "Ni wakati wa majaribu, taifa letu linasukwasukwa."

Kanisa Katoliki (RC) kupitia kwa maaskofu hao linasema kuwa tangu Juni 13, 2022, maeneo kadhaa ya Kivu Kaskazini, kama vile Bunagana, Rutshuru and Kiwanja "yametwaliwa tena na waasi wa M23."

Wanasema kuwa, "kwa mujibu wa taarifa kutoka vyanzo vya uhakika," waasi hawa wanapata msaada wa kijeshi kutoka nchi jirani za Rwanda na Uganda."

Aidha, maaskofu hao wameyataja matukio ya wananchi wa Kongo Kati, kwenye maeneo ya Kimpangu, Mbanza-Ngungu na Sona-Bata, kufukuzwa kwenye vijiji vyao, nyumba zao kuteketezwa, na makaburi kuharibiwa, kwa sababu ya madai kwamba, tayari "ardhi yao inauzwa kwa wageni wasiofahamika."

"Taifa letu liko hatarini, kiasi kwamba, tusipokaa chonjo, siku moja tutaamka na kukuta nchi yetu imemegwa vipande,lazima tuwe macho," maaskofu wa Cenco wanaonya.

Maaskofu hao pia wamelaani "unafiki wa jumuia ya kimataifa" kwa madai kwamba wanaziacha huru Rwanda na Burundi zinazosababisha matatizo haya, na badala yake kuwawekea vikwazo waasi



*Rais wa DRC Felix Tshisekedi*

wa M23 pekee ambao ni mawakala wa serikali hizo.

"Kuna hatari kubwa ya nchi yetu kumeguka. Kwa hiyo, ni jukumu la kila mmoja wetu kubeba jukumu la kiraia la kulinda nchi bila kujali tofauti zetu za kisiasa," wanasema maaksofu hao wa DRC.

"Tunawaalika Wakristo na watu wenye mapenzi mema kufunga, kusali na kuonyesha mshikamano na watu waliogeuzwa wakimbizi ndani ya nchi yao, kwa kushiriki maandamano ya amani yatakayofanyika nchi nzima Desemba 4, 2022," waraka wa maaskofu wa DRC unaelekeza.

Kikundi cha waasi wa M23 kinataka kuunda dola huru katika upande wa mashariki mwa DRC, dola wanayotaka iitwe "North Kivu State."

Inadaiwa kuwa eneo hili ni makazi ya kabila la Banyamulenge, ambao ni "Watusi wa Kongo," wenye undugu na "Watusi wa Rwanda."

Kikundi cha M23 kilianzishwa Aprili 4, 2012, baada ya wanajeshi 300 kuasi dhidi ya Jeshi la DRC, wakipinga kitendo cha serikali kushindwa kutekeleza makubaliano ya Machi 23, 2009 yaliyoelekeza kuwepo mgawanyo sawa wa nafasi za juu za uongozi.

# FIFA yakamiwa kulipa fidia waliokufa




**Na Mwandishi WETU**

SHIRIKISHO la Soka Duniani (FIFA) limetumbukia katika shinikizo kubwa kutoka mashirika ya kutetea haki za binadamu yakitaka kulipwa fidia stahiki kwa familia za watu waliopoteza maisha wakati wa ujenzi wa miondombinu ya kuandaa michuano ya Kombe la Dunia iliyoanza jana nchi Qatar.

Taarifa zinaeleza kuwa mashirika hayo makubwa duniani ya kutetea haki za bindamu yanataja kuwepo kwa watu 6,500 waliofariki dunia kutokana na kupata ajali na kuteswa wakati wa ujenzi wa viwanja, hoteli, mabarabara, uwanja wa ndege na miundombinu nyingine.

Inadaiwa kuwa ndani ya miaka mitatu na miezi saba, sawa na miezi 45, wastani wa watu 12 walikuwa wakipoteza maisha katika ujenzi wa miundombinu ndani ya miji ilikopangwa kufanyika michuano hiyo inayoshirikisha timu za soka za wanaume kutoka mataifa 32.

Tayari mtandao maarufu wa kutetea haki za binadamu, Avaaz umeanza kampeni hiyo kwa kuhimiza watu wote "wenye mapenzi mema" kusaini andiko lao ili kuliwasilisha FIFA kwa ajili ya utekelezaji wa kulipa fidia hizo.

Mashirika mengi ya kutetea haki za binadamu mara baada Qatar kutangazwa kuwa mwenyeji wa michuano hiyo, yalipinga kwa maelezo kwamba nchi hiyo ina rekodi mbaya ya kutozingatia haki za binadamu.

Qatar imekuwa ikidaiwa kuwa miongoni mwa nchi za Kiarabu zisizozingatia haki za binadamu, hasa kwa wafanyakazi wanaotoka nje ya nchi hiyo.

Nchi hiyo yenye idadi ya watu wanaoelezwa kufikia milioni 2.6, ina idadi ndogo zaidi ya raia na inakadiriwa kuwa wako asilimia 15 tu ya idadi hiyo ya watu.

Inaelezwa kuwa FIFA imekuwa ikisita kuanza mchakato au kushinikiza Qatar na kampuni husika, kuanza kulipa fidia kwa waliopoteza maisha kwa kuhofia "kufilisika."

Pamoja na shirikisho hilo la soka kusita kulipa, kampuni kubwa nne ambazo ni wafadhili wa michuano ya mwaka huu; Budweiser, McDonalds, Coca Cola, na Adidas zimeonyesha kukubali kulipwa fidia kwa wote waliofariki dunia kutokana na kuhusika katika maandalizi ya kinyang'anyiro hicho.

Avaaz inaeleza kuwa kuna idadi kubwa ya mashabiki wanaohudhuria na wale wanaofuatilia kutoka mbali, kuunga mkono shinikizo la kuwafidia wafanyakazi waliofariki dunia.

# PAMBAZUKO KUSHABIKIA GHANA




*Hawa ni baadhi ya mashabiki wa Timu ya Taifa ya Soka ya Ghana ambayo inashiriki michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar iliyoanza jana. Pambazuko linatangaza rasmi kwamba linashabikia timu hiyo na litatoa ushirikiano kwa kila linalowezekana ili timu hiyo ishinde. Ghana inatua uwanjani Alhamisi katika mechi yao ya kwanza dhidi ya Ureno. Tunaitakia kila heri. (Picha kutoka Pulse)*

*GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION